Tangazo la Serikali Na..... la Tarehe.............

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA, SURA YA 290

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 6(1) na 16(1)*

## SHERIA NDOGO ZA (UDHIBITI WA VYOMBO VYA USAFIRI NA UBORESHAJI WA MAPATO) ZA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM ZA MWAKA 2019

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina na Tarehe ya kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za (Udhibiti wa Vyombo vya Usafiri na Uboreshaji wa Mapato) za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam za Mwaka 2019 na zitatumika baada ya kutangazwa katika gazeti la Serikali.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo la mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:-

*"Ada na ushuru"* maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri au wakala wake kwa ajili ya huduma, vibali, au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

*"Afisa Mwidhiniwa"* Maana yake ni Afisa yeyote wa Halmashauri atakayeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

*"Chombo cha Usafiri"* maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha Mtu, Watu au mizigo kutoka sehemu moja kwenda nyingine isipokuwa Wanyama, Mikokoteni na Baiskeli;

*“Magari ya mizigo”* maana yake ni magari yanayobeba mizigo yenye uzito zaidi ya tani moja na nusu (Kilogram 1500);

“*Halmashauri”* Maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

*“Jiji”* Maana yake Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

*“Kituo cha Mabasi”* maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kuidhinishwa na Halmashauri kwa madhumuni ya kupakia na kuteremsha abiria na mizigo ya Abiria;

*“Mtumiaji wa kituo“* maana yake ni mtu yeyote anayefanya shughuli zake za kila siku ndani ya kituo na ametambuliwa na Halmashauri;

*“Abiria“* maana yake ni mtu yeyote mwenye nia ya kusafiri au kupata huduma ya usafiri ndani ya kituo;

*“Katikati ya Jiji (Central Business District (CBD) na Kariakoo Business District (KBD))”* maana yake ni eneo lote la katikakti ya mji kuanzia Salender Bridge, Barabara ya Umoja wa Mataifa hadi Kituo cha Zima moto (fire station), barabara ya Morogoro hadi BRT Jangwani, kuelekea barabara ya Kigogo kupitia jangwani, barabara ya Kawawa hadi makutano ya barabara ya Julius K. Nyerere, Njia panda ya Kamata hadi mzunguko (round about) wa Bandari na Bahari ya Hindi.

*“Maegesho’’* Sehemu yeyote iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuegesha vyombo vya usafiri kwa muda;

*“Manispaa”* Maana yake ni Halmashauri za Manispaa zinazounda Jiji la Dar es salaam kwa mujibu wa Sheria.

*“Mkurugenzi”* maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam au Afisa yeyote wa umma atakayeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

*“Ushuru*” maana yake ni tozo au malipo yatakayolipwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

## SEHEMU YA PILI
## UDHIBITI WA VYOMBO VYA USAFIRI

Wajibu wa Halmashauri

4. Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuweka utaratibu wa usimamizi na matumizi ya barabara, vituo vya mabasi na maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya maegesho ya magari.

Marufuku ya kuingia katikati ya Jiji

5. (1) Itakuwa ni marufuku kwa magari ya mizigo, pikipiki ya magurudumu mawili au matatu, matoroli au maguta kuingia katikati ya Jiji kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5 (1) magari ya mizigo, pikipiki ya magurudumu mawili au matatu yanaweza kuingia katikati ya Jiji baada ya kupata kibali kutoka Halmashauri.

(3) Kibali cha kuingia katikati ya Jiji kitatolewa baada ya mwombaji kujaza fomu ya maombi na kulipia ada kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Kwanza** la Sheria Ndogo hizi.

(4) Magari ya taka na mitambo yoyote hayataruhusiwa kuzoa au kukusanya taka au kufanya kazi katikati ya Jiji nyakati za mchana isipokuwa kwa dharura, kwenye maeneo maalum ya kukusanyia taka (transfer station) au kwa kibali maalum cha maandishi kutoka Halmashauri.

## SEHEMU YA TATU
## VITUO VYA MABASI

Wajibu wa kuanzisha Vituo vya mabasi

6. Itakuwa ni wajibu wa Halmashauri kuanzisha vituo vya mabasi yanayofanya shughuli za kusafirisha abiria na mizigo kwa kuanzia na kumalizia safari zake za mikoani na nchi jirani ndani ya Halmashauri.

Wajibu wa kutumia vituo vya mabasi

7. Itakuwa ni Marufuku kwa mtu yeyote au mmiliki wa chombo cha usafiri kuanzisha kituo cha mabasi, kushusha, kupakia abiria au mizigo katika eneo ambalo halijatengwa au kutambuliwa kwa kupewa kibali na Halmashauri kwa ajili ya kituo cha mabasi.

Orodha ya Watumiaji wa Kituo cha Mabasi

8. (1) Halmashauri itaweka utaratibu wa kuwatambua watumiaji wa kituo cha mabasi kwa mujibu wa vyama au vyombo vilivyosajiliwa na kutambulika na Sheria za Nchi na kuandikishwa na Halmashauri.

(2) Watumiaji wa kituo wanaofanya shughuli zao ndani ya kituo watatambulika kwa vitambulisho na watalazimika kuvaa vitambulisho hivyo vilivyotolewa na Halmashauri wakati wote wawapo kituoni.

(3) Halmashauri itatoza ushuru kwa watumiaji wa Kituo cha mabasi kama ilivyoainishwa katika **Jedwali la Pili (2)** la Sheria Ndogo hizi.

Ushuru wa maegesho vyombo vya usafiri

9. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa vyombo vya usafiri kwa ajili ya maegesho katika maeneo yaliyotengwa, kuingia katika kituo cha mabasi, kulaza gari na kuegesha gari ndani ya stendi kwa mujibu wa viwango vilivyoainishwa katika **Jedwali la Pili (2)** la Sheria ndogo hizi.

(2) Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuingia eneo lolote kwa wakati wowote ndani ya kituo cha mabasi kwa ajili ya kutoza ushuru au kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii.

Kodi ya pango ya eneo la matangazo ya biashara

10. (1) Halmashauri itatoza kodi ya pango (rental fees) ya eneo la kuweka bango la matangazo katika eneo lolote ndani au kuzunguka nje ya kituo cha mabasi kwa mujibu wa viwango vitakavyoelekezwa na Halmashauri kulingana na vipimo vya bango husika.

(2) Bila kuathiri kifungu cha 11 (1) Halmashauri itatoza kodi ya matangazo ndani ya kituo kwa mujibu wa viwango vitakavyoelekezwa na Halmashauri kulingana na aina ya tangazo husika.

Usafi wa Mazingira

11. (1) Ni wajibu wa kila Mtumiaji wa kituo cha mabasi kuhakikisha kuwa anatunza mazingira kwa kutotupa taka ovyo za aina yoyote au kutiririsha maji katika eneo la kituo cha mabasi.

(2) Kila mmiliki wa basi atahakikisha kuwa anaweka chombo cha kutupia na kutunza taka ndani ya basi na kutupa taka hizo katika maeneo maalum ndani ya kituo cha mabasi.

(3) Ni marufuku kwa Mtu yeyote kutupa taka ovyo, kumwaga au kutiririsha maji ovyo, kuosha vyombo vya usafiri katika vituo vya mabasi isipokuwa katika eneo lililotengwa kwa

ajili hiyo.

## SEHEMU YA NNE
## MAEGESHO YA MAGARI JIJINI

Maeneo ya Maegesho

12. (1) Halmashauri itashauriana na Mamlaka nyingine katika kutenga maeneo kwa ajili ya maegesho ya magari binafsi, taxi na malori au vyombo vingine vya usafiri.

(2) Halmashauri itaweka alama au michoro maalum itakayoonesha maeneo ya maegesho au namna yoyote ile itakayoashiria eneo la maegesho ya magari au chombo kingine cha usafiri.

(3) Mtu yeyote, Kampuni au Shirika au Kikundi ambacho kitanzisha eneo au maeneo kwa ajili ya maegesho kitapaswa kuwa na kibali kutoka Halmashauri na kitapaswa kulipia maegesho hayo kwa mujibu wa makubaliano baina yake na Halmashauri.

(4) Maeneo ya maegesho yatafunguliwa kuanzia saa moja na dakika thelathini asubuhi (1:30) hadi saa kumi na moja jioni (11.00) katika maeneo ya kawaida na kuanzia saa moja na dakika thelathini asubuhi (1:30) hadi saa nne usiku (4.00) katika maeneo ya fukwe za bahari.

Ushuru wa maegesho

13. (1) Halmashauri itatoza ushuru wa maegesho kwa mujibu wa viwango vilivyowekwa katika **Jedwali la Tatu (A)** la Sheria Ndogo hii.

(2) Halmashauri inaweza kutoa kibali kwa ajili ya maegesho katika maeneo maalum ***"Reserved area"*** endapo Mwombaji atalipa ushuru wa maegesho kwa kipindi cha kuanzia wiki moja.

(3) Halmashauri itatoa stakabadhi ya uthibitisho wa malipo ya ushuru wa maegesho kwa Mtumiaji wa chombo cha usafiri kulingana na muda alioutumia kuegesha chombo chake cha usafiri.

(4) Mtu yeyote atakayelipia ushuru wa maegesho kwa jumla ya gharama za siku, wiki au mwezi kwa mkupuo atapewa kibali maalum kitakachomruhusu kuegesha katika eneo lolote lililotengwa na Halmashauri kwa maegesho bila malipo.

Maegesho yasiyo rasmi ***(Wrong parking).***

14. (1) Itakuwa marufuku kuegesha gari au chombo chochote cha usafiri katika maeneo yasiyotengwa kwa ajili ya maegesho, au kuegesha kwa namna isiyoruhusiwa *(wrong parking).*

(2) Halmashauri italikokota au italizuia kwa kulifunga vifaa maalum gari au chombo cha usafiri kilichoegeshwa isivyoruhusiwa au kilichoegeshwa katika eneo lisiloruhusiwa na kumtaka Mmiliki au mtumiaji kulipa faini na kuliondosha gari hilo.

Gharama za Uondoaji na Uvutaji wa magari

15. (1) Halmashauri au Wakala atatoza gharama ya uvutaji, utunzaji pamoja na gharama zingine zitakazojitokeza wakati wa kukamata chombo cha usafiri kilichoegeshwa vibaya au kinyume cha matakwa ya Sheria Ndogo hizi.

(2) Gharama za uondoaji, uvutaji na utunzaji wa vyombo vya usafiri zitakuwa ni kama zilivyoainishwa kwenye **Jedwali la Tatu (B)** la Sheria Ndogo hizi.

(3) Pale ambapo gari halitachukuliwa kwa zaidi ya mwezi mmoja Halmashauri itauza kwa njia ya mnada wa hadhara baada ya kupata idhini ya mahakama.

(4) Halmashauri itatumia mapato yaliyopatikana katika kifungu cha 16 (4) kulipia gharama ilizotumia na kiasi kilichobakia kitarejeshwa kwa mmiliki.

Msamaha wa kulipa ushuru wa Maegesho

16. (1) Halmashauri haitatoza ushuru wa maegesho kwa vyombo vya usafiri vifuatavyo;-
(a) Magari ya Serikali;
(b) Magari ya Kibalozi;
(c) Magari yaliyoegeshwa katika sehemu za Ibada *(muda wa ibada)*;
(d) Magari yaliyo na vibali maalumu kutoka Halmashauri;
(e) Magari yaliyoegesha katika maeneo ya maegesho wakati wa shughuli maalum za kitaifa; na
(f) Magari ya wagonjwa, taka na zimamoto.

Makosa na Adhabu

17. Itakuwa ni kosa kwa Mtu yeyote endapo;

(a) Atamzuia Afisa Mwidhiniwa au Wakala wa Halmashauri

kutekeleza majukumu yake ya kusimamia Sheria Ndogo hizi;

(b) Ataharibu kwa namna yoyote miundombinu ya barabara, vifaa, kamera za usalama au taa za barabarani katika maeneo ya maegesho na kituo cha mabasi;

(c) Ataegesha chombo cha usafiri katika maeneo yasiyo rasmi kwa maegesho *(wrong parking);*

(d) Atabughudhi abiria, atapiga debe au kutoa maelekezo yoyote bila idhini ya Halmashauri,

(e) Atakataa, atashindwa au atashawishi mtu yeyote kutokulipa viwango vya ada na ushuru vilivyoainishwa na Sheria Ndogo hizi;

(f) Ataingiza gari la kuzoa taka, au kufanya kazi ya kukusanya taka katikati ya Jiji nyakati za mchana isipokuwa kwa dharura na kibali cha maandishi kutoka kwa Mkurugenzi;

(g) Ataingia au kutumia kituo cha mabasi pasipo kulipia ushuru husika;

(h) Atalaza, ataosha au atatengeneza chombo cha usafiri, au atafanya shughuli yoyote kwenye eneo lolote ambalo halijatengwa kwa shughuli hiyo ndani Kituo cha mabasi;

(i) Atachafua mazingira kwa kutupa taka za aina yoyote ndani ya kituo cha mabasi au atatupa taka kutoka kwenye chombo cha usafiri;

(j) Atatumia lugha ya matusi, zenye kuleta uchochezi na kubughudhi zinazohatarisha usalama na amani ndani ya kituo.

(k) Atatenda jambo lolote ambalo ni kinyume cha Sheria Ndogo hizi;

Adhabu

18. Mtu yeyote atayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na endapo atapatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua Shilingi Laki Mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi Milioni Moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua Miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi Ishirini

na Nne au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

19. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa endapo Mkosaji atakiri kosa kwa hiari yake mwenyewe na kukubali kulipa faini kiasi kisichopungua Shilingi Laki Mbili (200,000/=) na kisichozidi shilingi Laki Tano (500,000/=) baada ya kujaza fomu iliyoainishwa katika **Jedwali la Nne (4)** pamoja na kulipa kiasi cha ushuru anaodaiwa.

Kufutwa Tangazo la Serikali Na. 41 la tarehe 24/02/2017

20. Sheria Ndogo za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Udhibiti wa Vyombo vya Usafiri na Uboreshaji wa Mapato) za Mwaka 2017 zinafutwa.

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limeundwa Chini ya Kifungu cha 5)*

### (A) VIBALI VYA PIKIPIKI NA BAJAJI

| NA. | MUDA WA KIBALI (MWEZI) | ADA (TSH) |
|---|---|---|
| (A) | PIKIPIKI | |
| 1. | 1 - 3 | 60,000/= |
| 2. | 4 - 6 | 100,000/= |
| 3. | 7 - 12 | 180,000/= |
| (B) | BAJAJI | |
| 4 | 1 - 3 | 80,000/= |
| 5 | 4 - 6 | 120,000/= |
| 6 | 7 - 12 | 200,000/= |

### (C) VIBALI VYA GARI ZA MIZIGO

| NA. | UZITO WA GARI YA MIZIGO | ADA YA KIBALI KWA SIKU (TSH) |
|---|---|---|
| 1. | Tani 2 hadi tani 3.5 | 20,000/= |
| 2. | Tani 4 hadi tani 10 | 50,000/= |
| 3. | Zaidi ya tani 10 | 100,000/= |

## JEDWALI LA PILI (A)

*(Limeundwa Chini ya Kifungu cha 8)*

## USHURU WA KUTUMIA VITUO VYA MABASI

| Na. | Aina ya Chombo | Ushuru |
|---|---|---|
| 1. | Basi Dogo la abiria kati ya 1 – 20 | 2,000 kila linapoingia |
| 2. | Basi kubwa la abiria kati ya 20 – 28 | 5,000 kila linapoingia |
| 3. | Basi kubwa la abiria zaidi ya 28 | 10,000 kila linapoingia |
| 4. | Gari Dogo (Taxi Cab) | 1,000 kila linapoingia |
| 5. | Gari Dogo (Binafsi) | 1,000 kila linapoingia |
| 6. | Magari ya Mizigo (Pick-up) | 4,000 kila linapoingia |
| 7. | Magari ya Mizigo yasiyozidi tani 3 | 5,000 kila linapoingia |
| 8. | Magari ya Mizigo yanayozidi tani 3. | 10,000 kila linapoingia |
| 9. | Pikipiki | 500 kila linapoingia |
| 10. | Magari mengine | 1,000 kila linapoingia |
| 11. | Baiskeli | 500 kila inapoingia |
| 12. | Ada ya Kuingia mtu mmoja | 300 kila anapoingia |
| 13. | Kufunga magari | 30,000 kwa gari |
| 14. | Huduma za choo | 300 |
| 15 | Huduma za bafu (kuoga) | 500 |

## JEDWALI LA PILI (B)

*(Limeundwa Chini ya Kifungu cha 9)*

## USHURU WA MAEGESHO USIKU (KULAZA GARI)

| Na. | Aina ya Chombo | Ushuru kwa usiku mmoja (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa la abiria kati ya 20-28 | 4,000 |
| 2. | Basi kubwa la abiria 28 | 5,000 |
| 3. | Basi Dogo la abiria kati ya 1-20 | 3,000 |
| 4. | Gari Dogo (Taxi Cab) | 3,000 |
| 5. | Gari Dogo (Binafsi) | 1,000 |
| 6. | Trucks na Trailers zaidi ya tani 3 | 5000 |
| 7. | Trucks na Trailers tani 3 na zaidi | 10,000 |
| 8. | Magari ya Mizigo (Pick-up) | 3,000 |
| 9. | Magari mengine | 3,000 |
| 10. | Pikipiki | 1,000 |
| 11. | Baiskeli | 1,000 |

## JEDWALI LA TATU (A)

*(Limeundwa Chini ya Kifungu cha 13)*

## USHURU WA MAEGESHO KATIKA MAENEO YALIYOTENGWA

| Na. | Muda | Kiwango (Tsh) |
|---|---|---|
| 1. | Maegesho katikati ya Jiji **(CBD** na **KBD)** na fukwe za bahari | 500/= kwa saa moja,<br>4,500/= kwa siku,<br>135,000/= kwa Mwezi, |
| 2. | Maegesho ya pembezoni ya Jiji | 300/= kwa saa,<br>2,000/= kwa siku,<br>60,000/= kwa Mwezi, |

## JEDWALI LA TATU (B)

*(Limeundwa Chini ya Kifungu cha 15)*

## GHARAMA ZA UONDOAJI, UVUTAJI NA UTUNZAJI WA MAGARI

| NA. | AINA YA GARI | ADA | UTUNZAJI |
|---|---|---|---|
| 1 | Basi kubwa la abiria zaidi ya 28 | 400,000/= | 20,000/= |
| 2 | Basi Dogo la abiria chini ya 28 | 300,000/= | 20,000/= |
| 3 | Gari Dogo (Taxi Cab) | 80,000/= | 20,000/= |
| 4 | Gari Dogo (Binafsi) | 80,000/= | 20,000/= |
| 5 | Lori na Tela chini ya tani 3 | 300,000/= | 20,000/= |
| 6 | Lori na Tela tani 3 na zaidi | 400,000/= | 20,000/= |
| 7 | Magari ya Mizigo (Pick-up) | 100,000/= | 20,000/= |
| 8 | Magari mengine | 100,000/= | 20,000/= |
| 9 | Pikipiki | 20,000/= | 20,000/= |
| 10 | Baiskeli | 20,000/= | 10,000/= |

## JEDWALI NAMBA NNE

## HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

*(Chini ya kifungu cha 19)*

Mimi ………………………………..………mkazi wa Mkoa wa …………………….. nakiri mbele ya …………………….…………..ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, kwamba mnamo tarehe …… ya Mwezi ……. Mwaka 20….… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za (Udhibiti wa Vyombo vya usafiri na Uboreshaji wa Mapato) za Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam za Mwaka 2019.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurgenzi wa Jiji, Niko tayari kulipa kiasi cha …………………… ninachodaiwa kama faini na hasara niliyosababisha.

**NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU**

Leo tarehe ……………….Mwezi ………………………..Mwaka, ………………

Jina: ………………………………………………. Saini: ……………………….

**Mbele ya**: *(Afisa aliyemkamata mtenda kosa)*

Jina: ………………………………………………. Saini: ……………………….

**TAMKO LA MKURUGENZI**

Kwa mamlaka niliyopewa na Sheria Ndogo nafifilisha kosa lako na kukuamuru Ndugu ………………………………………………….. kulipa faini ya shilingi za kitanzania ……………………………..………………. (Tshs. ………………..) ikiwa ni adhabu kwa mujibu wa kifungu cha …………….. cha Sheria Ndogo hizi TS. Na. ………./20……

Jina: ………………………………………..

Saini: ……………………………………… (*muhuri)*

Cheo: ……………………………………….